











Maelezo ya kifaa saidizi	Kinafaa kwa watu	Muonekano wa kifaa saidizi	
<p><b>Chuma cha kushikilia:</b> Chuma kilicho kwenye ukuta ambacho mtu anaweza kushikilia ili aweze kusima bila kutetereka na kumsaidia kusogea.</p>	<p>Kinafaa kwa watu ambao wanahitaji msaada zaidi wakati wanapotaka kusogea kwenda chumbani, bafuni, uani au kwenye ngazi.</p>		
<p><b>Kifaa saidizi cha kupandia ngazi kinachobebeka:</b> Kifaa saidizi kinachobebeka hakifungwi sehemu moja na kinaweza kupelekwa kwingine inapohitajika kufanya hivyo.</p>	<p>Kinafaa watu ambao wanatumia kiti cha magurudumu, Rolata au fremu ya kutembelea na wanahitaji kwenda kwenye maeneo mengine yenye ngazi.</p>		
<p><b>Viatu vinavyofaa:</b> Viatu vinapatikana kwenye maeneo ambayo mtu anaishi, vinamkaa vizuri mvaaji na vina vitu vya kuweza kuulinda mguu na kupunguza uwezekano mtu kuanguka.</p>	<p>Ni muhimu kwa watu walio katika hatari ya kuanguka, ambao wanatumia kifaa saidizi cha kutembelea, au wako katika hatari ya kupata kidonda.</p>		
<p><b>Viatu tiba:</b> Viatu vyenye vitu ambavyo vinaweza kulinda na kusaidia miguu.</p>	<p>Mtu anayehitaji hivi viatu zaidi ni yule mwenye hatari ya kati au kubwa ya kupata kidonda</p>		
<p><b>Ubao unaomsadia mtu kuhama kutoka sehemu oja kwenda sehemu nyingine:</b> Ubao saidizi unaweza kumsaidia mtumiaji kusogea kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.</p>	<p>Unamfaa mtu mwenye taabu kusimama au aliyebeba uzito kwenye miguu yake.</p>	<p>Ubao uliopinda</p>  <p>Ubao ulionyooka</p> 	

<p><b>Vifaa saidizi vya kutembelea:</b> Vifaa saidizi vinavyowasaidia watu kusimama, kukaa na kutembea.</p>	<p>Kuna aina tofauti ya vifaa saidizi ambavyo vinaendana na mahitaji ya watu</p>	 <p>Rolato</p>	 <p>Magongo</p>
<p><b>Vifaa saidizi vya kusaidia mguu kutembea:</b> Ni kifaa saidizi ambacho kinasaidia sehemu ya kiungo cha binadamu. Vifaa hivi hugawiwa kupitia huduma za utengamo au viungo bandia.</p>	<p>Aina tofauti za vifaa saidizi ambavyo vinafaa watu wenye mahitaji tofauti</p>	 <p>Kifaa saidizi cha goti</p>	 <p>Kifaa saidizi cha kifundo cha mguu</p>
<p><b>Mguu bandia:</b> prosthetist. Unatu mika kufanya kazi ya mguu wa mtu ambao umekatwa. Mara nyingi mguu bandia unatengenezwa ili umtoshe mtumiaji. Unatengenezwa na mtu aliyefuzu mafunzo</p>	<p>Unafaa watu ambao wamekatwa mguu au wana sehemu ya mguu inayokosekana. Sio kila mtu ambaye hana sehemu ya mguu anaweza kutumia mguu bandia.</p>	 <p>Mguu bandia unaoanzia sehemu ya chini ya goti.</p>	 <p>Mguu bandia unaoanzia sehemu ya juu ya goti.</p>
<p><b>Fremu ya kutembelea inayowekwa nyuma ya mtumiaji:</b></p> <p>Ni fremu inayomsaidia mtoto kutembea kwa nyuma. Mara nyingi inaweza kutumika pamoja na vifaa saidizi vingine kama viungo bandia vya kwenye mguu ambavyo vinatolewa na kituo mazoezi ya viungo.</p>	<p>Kinafaa kwa watoto wenye mtindio wa ubongo</p>		
<p><b>Kifaa saidizi cha kusimama na kulala</b></p>	<p>Kinasaidia kuzuia matatizo ya kiafya kwa watoto na watu wazima ambao wanapata taabu kulala na kusimama kwa usalama bila ya kuwa na msaada.</p>	 <p>Fremu ya kusimama</p>	 <p>Kifaa saidizi cha kulala</p>

<p><b>Kiti chenye magurudumu:</b> Mpe kifaa saidizi cha kusogea chenye sehemu ya kukaa.</p>	<p>Kinatumiwa na watu ambao hawawezi kutembea au ambao wanapata taabu kutembea. Aina tofauti ya viti vyenye magurudumu vinaweza kukithi mahitaji ya watu tofauti.</p>	
---	---	--

**Kumbuka: Kwa vitu vyote hivi, nimuhimu kufuata hatua zote nne za ugawaji wa vifaa saidizi**



Hatua ya kwanza -  
Tathmini



Hatua ya pili – Kupata  
kipimo sahihi



Hatua ya tatu - Kutumia



Hatua ya nne – Kufanya  
ufatiliaji